BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Tisa – Tarehe 24 Februari, 2025.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

179. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa PIli wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kumekuwa na malalamiko mengi yanayohusiana na maslahi ya Polisi Zanzibar.

(a) Je, kikokotoo cha maslahi ya Polisi wanaostaafu Zanzibar kinatofautiana na vikokotoo vya wastaaafu wengine.

(b) Je, ni upi utaratibu wa kuwafidia haki zao askari Polisi wanaomaliza kozi wakiwa kazini na wanaosubirishwa kwa muda mrefu bila ya kupandishwa vyeo.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

72. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi na utawala Bora:

Upatikanaji wa ajira nchini mwetu umekuwa ni tatizo ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi unaostahiki hasa kwa walimu.

(a) Je, Serikali imetoa vipaumbele gani kwa ajira za walimu nchini.

(b) Je, Serikali inawaeleza nini walimu hao.

(c) Je, ni walimu wangapi wamepata ajira hizo kutoka jimbo la Paje.

176. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali imechukua juhudi kubwa kuwasomesha watumishi ambao tayari wako kazini. Hata hivyo, kumekuwa na wasiwasi kati ya taaluma inayopatikana kulinganisha na muda na fedha inayotumika.

(a) Je, Serikali inatumia vigezo gani kuhakikisha kwamba watumishi wanaopelekwa kusoma hawapelekei kupoteza fedha nyingi ya Serikali ukilinganisha na matokeo ya elimu inayopatikana.

(b) Je, Serikali inafuatilia vipi umakini “seriousness” wa wanafunzi watumishi wakiwa masomoni.

(c) Je, ni vipi vigezo na utaratibu wa sasa kwa watumishi wanaopelekwa masomoni.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

23. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika kukabiliana na changamoto za ajira hususani kwa vijana.

Serikali imechukuwa hatua gani katika kuhakikisha inawakwamua vijana kiuchumi.

<u>**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**</u>

149. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na kampeni mbali mbali za kuimarisha suala la usafi wa mazingira katika Halmashauri zetu huku kukiwa na kauli mbiu mbali mbali.

(a) Je, kauli mbiu ngapi zimetumika katika Halmashauri zetu katika suala zima la kupambana na usafi wa mazingira.

(b) Je, ni kwa kiasi gani kauli mbiu hizo zimeweza kuleta matokeo chanya.

(c) Je, ni ipi kauli mbiu mpya kwa sasa inayohamasisha kupambana na usafi wa mazingira.

<u>**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**</u>

168. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

(a) Kuna watoa huduma wangapi wa kifedha waliosajiliwa na kusimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania.

(b) Tathmini iko vipi juu ya utekelezaji wao wa majukumu kwa mujibu wa kanuni.

(c) Kwa kiasi gani elimu ya fedha inapewa mazingatio na kwa taratibu gani malalamiko ya wateja wa huduma za kifedha huwa yanapatiwa ufumbuzi kati ya taasisi za kifedha na wateja wao.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

35. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Ni lini Wizara yako itaboresha huduma za msingi kwa watalii katika maeneo ya vivutio wanavyovitembelea ikiwemo huduma za vyoo vya kisasa, maji safi, huduma ya mitandao hasa katika maeneo ya nje ya miji yetu.

36. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    (a) Tuna vyuo na taasisi ngapi nchini zinazotambulika ambazo zinatoa mafunzo ya ukarimu na utalii.

    (b) Kwa kiasi gani mafunzo yanayotolewa kwenye vyuo na taasisi hizi yanakidhi malengo na matakwa ya watalii na manufaa ya taifa kwa ujumla.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

112. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

     Ni ipi tathmini ya mafanikio ya ziara yako nchini Cuba katika maendeleo ya lugha yetu adhimu ya Kiswahili.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

83. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Hospitali ya kutibu wanyama na mifugo iliyopo Mbweni, inakabiliwa na changamoto tofauti.

    Je, Wizara imechukua hatua gani ya kuzitatua changamoto hizo.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

74. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa maji katika shehia ya Kitogani na Muungoni kutokana na mashine ya Kitogani kuharibika.

(a) Je, kuanzia lini Wizara yako imelifahamu tatizo hilo.

(b) Je, ni lini mashine hiyo itatengenezwa na kuanza tena kufanya kazi.

(c) Je, Wizara yako inatoa kauli gani kwa wananchi wa shehia hizo ambao wameshavumilia kwa muda mrefu sasa.

## Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

191. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kila inapofika mwezi Mtukufu wa Ramadhani Serikali inatoa maelekezo mengi kwa wafanyabiashara ikiwemo bei elekezi ya vyakula muhimu ili kuwapatia unafuu wananchi waweze kumudu kununua biadhaa muhimu za vyakula. Pamoja na jambo hili tumekua tukiona wafanyabiashara wakipandisha bidhaa na kutokufuata maelekezo kisingizio kikiwa ni utitiri wa tozo na kodi wanazotozwa na Serikali.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa kwa bei nafuu katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani ya mwaka huu 2025.

(b) Je, Serikali haioni kuna haja yakuwa na mpango maaluum wa kupunguza tozo na kodi kwa wafanyabiashara ili kuweza kupunguza bei kwa mwananchi wenye kiwango cha chini katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

(c) Je, umefikia wapi ule mpango wa Serikali wa kuagiza bidhaa kama mchele ili kuweza kupunguza bei ya bidhaa hiyo muhimu katika kipindi cha mwezi wa Ramadhani.

**Wizara ya Afya:**

68. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Huduma katika hospitali ya Lumumba ikiwemo huduma za usafi zinaonekana kuanza kusuasua. Wafanyakazi katika hospitali hiyo wanapoulizwa huzipeleka lawama zao kwa Kampuni ya NSK inayoendesha hospitali hiyo.

(a) Je, Serikali yetu inalitambua vipi tatizo hili.

(b) Ni nani hasa anaehusika na huduma ya usafi kati ya Serikali au watu binafsi.

140. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi inastahiki pongezi kwa kazi kubwa na nzuri ya kuimarisha miundombinu katika sekta ya afya hasa ujenzi wa hospitali za kisasa za Wilaya.

(a) Je, ni wastani wa wagonjwa wangapi kwa kila siku wanapokelewa kupitia hosptali zetu za Wilaya.

(b) Je, ni yepi mafanikio ya uwepo wa hospitali zetu za Wilaya na kwa kiasi gani Wizara inakidhi matakwa ya uwezo wa kuwahudumia wagonjwa ipasavyo.

(c) Je, ni wastani wa magonjwa aina gani yaliyoripotiwa kuongoza katika hospitali zetu za Wilaya kwa hivi karibuni.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

53. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Uwepo wa rasilimali ya maji bahari unawezesha utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Uchumi wa Buluu ikiwemo uvuvi, utalii na uchukuzi.

Ni kwa kiasi gani Wizara inashughulika na utatuzi wa changamoto za muingiliano wa watumiaji wa rasilimali ya maji bahari ikiwemo wavuvi na wakulima wa mwani, wachimbaji wadogo wa chumvi na wahifadhi wa mikoko, ili kutoathiri miradi ya kimkakati ya Uchumi wa Buluu.

55. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Uhaba wa miundombinu na teknolojia za kisasa za kukusanya taarifa na takwinu zinaweza kuathiri jitihada za kuikuza Sekta ya Uchumi wa Buluu.

Je, Wizara yako imechukua jitihada zipi katika kuona kwamba inaliwekea mkakati suala la tafiti, ili kuweza kupata taarifa za kina zitakazowezesha fursa za Uchumi wa Buluu kutumika ipasavyo.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

86. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni lini Wizara yako itaona umuhimu wa kurasimisha bandari ndogo ndogo (Bandari bubu) kwa kuzitambua, kuzijenga na kuziwekea utaratibu mzuri ili ziweze kuchangia mapato na kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao.

174. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo la kupongezwa kwa meli ya Flying Horse kuanza tena safari zake zikiwemo safari kati ya visiwa vya Unguja na Pemba. Hata hivyo, kuna wasiwasi wa utayari na usalama wa meli hiyo.

(a) Je, Serikali imethibitisha vipi utayari wa meli ya Flying Horse kiumadhubuti na kiusalama wa abiria, sambamba na ukali wa mkondo wa maji katika masafa kati ya Unguja na Pemba.

(b) Je, meli ya Flying Horse imefanyiwa matengenezo na mabadiliko yepi makubwa ili kuondoa hitilafu za kiufundi na kiusalama ilizokuwa nazo kabla ya kusimamisha safari zake.

(c) Je, ni vigezo gani hutumiwa na Serikali kuzizuia meli na boti zilizochakaa na zisizo salama katika kutoa huduma za kusafirisha abiria na mali zao.

## II. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC):</u>**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2024/2025.

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**

**Zanzibar,**
**24 Februari, 2025.**